Kwa nini afya siyo kipaumbele katika bajeti ya taifa 2011/12 .

Uchambuzi wa mgao wa bajeti ya 2011/2012 kwa ajili ya sekta ya afya.

Dondoo ya sera: 04/11

Suala:

Mchakato wa bajeti ya mwaka unatoa fursa ya kutathmini kama taarifa kwa umma kuhusu vipaumbele vya serikali vinafuatwa. Kwa mfano, katika miaka ya hivi karibuni serikali imeonyesha nia ya kutaka kupata thamani halisi ya fedha kadri inavyotoa bajeti yake ili kuweza kukabiliana na matumizi yasiyo ya lazima.

Uchambuzi huu wa bajeti ya sekta ya afya 2011/12 kwa ufupi unatoa malengo maalumu yanayo tathmini thamani ya fedha. Uchambuzi unapima jinsi rasilimali zilizopo zimeweza kugawanywa na kama mgawanyo huo utaweza kuleta mabadiliko katika sekta ya afya.

1. Kuna ujumbe gani muhimu kwa mwaka 2011/12?

Makisio yafuatayo yameangaliwa:

- Sekta ya afya haijapewa kipaumbele kwa wakati huu, tofauti na zile za miundombinu na elimu. Ongezeko la bajeti yake ni asilimia 0.3 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka jana.
- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW) imeongeza bajeti yake ya posho kwa asilimia 94.
- Zaidi ya hayo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imetenga shilingi milioni 214 kwa shughuli za kisiasa badala ya shughuli za afya.
- Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alitoa ripoti kamili.
- Pia wadau wa maendeleo wamesitisha michango yao katika bajeti ya Wizara ya Afya.

2. Je, bajeti ya Sekta ya Afya kwa mwaka 2011/12 ina ukubwa gani?

Jumla ya shilingi bilioni 1,209.1 zimegawanywa kwa sekta ya afya kwa mwaka 2011/12 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,205.9 kwa mwaka 2010/11. Hii inaonyesha ongezeko la asilimia 0.3. Mchango wa sekta ya afya kwa bajeti ya taifa ni asilimia 8.9 pekee, ambayo ni chini ya kiwango kwa asilimia 15 ya malengo ya Abuja.

Jedwali no.1 Mabadiliko ya mgawanyo katika sekta kwa mwaka wa bajeti 2011/12



Chanzo: Makisio ya matumizi ya umma 2011/12 sehemu. II & IV

3. Ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii?

Kwa mwaka 2011/12 wizara inapokea kiasi cha shilingi 584 bilioni ikilinganishwa na shilingi bilioni 678 kwa miaka iliyopita. Ikiwa ni nakisi ya asilimia 14.

Jedwali 1; matumizi ya Wizara ya Afya (MoHSW)

Fedha zilizotengwa	2010/2011	2011/2012
Bajeti ya matumizi ya kawaida	229,978,968,000	219,367,376,000
Bajeti ya Maendeleo	448,442,515,000	364,794,487,000
Jumla	678,421,483,000	584,161,863,000

Chanzo: Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Umma 2011/12 Vol. II & IV

Nakisi hii ya bajeti ina athari kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hasa katika kupanga jinsi itakavyotumia fedha kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Bajeti iliyopita imepunguzwa kwa asilimia 4.6 na kiasi cha sasa ni shilingi 219 bilioni. Bajeti ya maendeleo imepungua ghafla kwa asilimia 18.6 hadi shilingi 365 bilioni.

Jedwali 2.Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
Chanzo: Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Umma 2011/12 Vol. II & IV



4. Ni kwa kiasi gani serikali inachangia miradi ya maendeleo ya MoHSW?

Kama ilivyoonyeshwa katika jedwali namba 3, wadau wa maendeleo wanachangia katika shughuli zote za maendeleo.Kati ya shilingi 364 bilioni zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ya wizara hii, serikali inachangia kiasi cha shilingi 9,873 milioni pekee au zaidi ya asilimia 3 tu.

Moja ya madhara makubwa yatokanayo na kutegemea zaidi ufadhili/misaada kutoka nje katika shughuli za maendeleo ni kwamba miradi mikubwa ya maendeleo inaweza kufa pindi wafadhili hao wanapojitoa. Hivyo basi, uwajibikaji wa serikali unahitajika ili kuhakikisha kuwa hakuna mradi wowote unaohusiana na maendeleo ya afya utakaokosa fedha pindi wahisani au wafadhili watakaposimamisha michango yao.

Jedwali 3: Vyanzo vya Bajeti ya Maendeleo ya MoHSW
Chanzo: Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Umma 2011/12 Vol. II & IV

5. Ni kiasi gani MoHSW imetenga kwa ajili ya posho na marupurupu?



baadhi ya mapendekezo yametolewa na viongozi wa serikali kuhusu kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikijumuisha posho. Waziri wa fedha alisema katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2011 juni "Serikali itaendelea kusimamia matumizi kwa kusitisha utumiaji wa aina zote za vyombo vya usafiri…kushusha matumizi ya posho….kupunguza bei ya mafuta…kupunguza safari za ndani na nje…Kuhakikisha kuwa semina na mikutano inapunguzwa…." Tofauti na matarajio yetu wizara ya afya na ustawi wa jamii imeongeza mgawanyo wa posho kwa asilimia 94 kwa mwaka 2011/12.Hii iimeibua umakini tangu wizara ishindwe kufikia malengo iliyopewa na wizara ya fedha.

Jedwali 4 : Jumla ya fedha za matumizi zilizotengwa kwa ajili ya posho na marupurupu mengine ya MoHSW
Chanzo: Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Umma 2011/12 Vol. II & IV



6. Ni kwa kiasi gani bajeti imegawanywa kiufanisi?

Pamoja na kwamba serikali haina rasilimali za kutosha kufadhili miradi yake yote ya muhimu, bado inaendelea kutenga bajeti kwa shughuli zisizo na tija kwa wizara. Mathalan, wafanyakazi wa MoHSW kuhudhuria kipindi cha Bunge na kutembelea majimbo. Gharama za ziara hizo kwa ujumla ni shillingi 214 milioni, ambapo asilimia 60 ya bajeti hiyo ni posho. Ili kuzuia matumizi hayo ya aibu na yasiyo ya lazima wafanyakazi wote wa wizara ambao wanaohudhuria Bunge wanapaswa walipwe kutoka kwenye mfuko wa Bunge.

Ushiriki wakati wa kipindi cha Bunge

Kazi	Juma
Ushiriki wa wafanyakazi 5 wa DHS katika vikao vya bunge vya bajeti	9,830,000
Ushiriki wa wafanyakazi wa DPP katika vikao vya bunge vya bajeti	19,710,000
Ushiriki wa kazi za Bunge Dodoma	20,018,000
Ushiriki wa MoHSW jaji mkuu katika shughuli za bunge	26,850,000
Mawaziri 2 na wasaidizi 6 kutembelea Jimbo	26,928,000
Ushiriki wa mawaziri 2 na wasaidizi wa wizara 10	110,956,000
Jumla	**214,292,000**

Chanzo: MoHSW 2011/12 MTEF

7. Hitimisho

Kwa ujumla, bajeti na uchangiaji katika sekta ya afya umepungua. Pia tumegundua kwamba MoHSW inakabiliwa na upungufu au nakisi ya bajeti yake kwa asilimia 14; hii imetokana na uchangiaji mdogo wa fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Wakati Wizara ya Fedha imeahidi kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa mwaka wa fedha 2011/12, MoHSW imejiongezea bajeti ya marupurupu na posho kwa takriban mara mbili zaidi. Mbinu rahisi ya kujipatia posho iliyotumika ni kupitia kuongeza marupurupu kwa safari za kwenda bungeni.

8. Mapendekezo

- Serikali irejee na iheshimu maazimio ya Abuja kwa kutenga asilimia 15 ya bajeti yake kwa sekta ya afya.
- Hatua zaidi zinahitaji kuchukuliwa ili kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima yanayofanywa kupitia posho na marupurupu.
- Shughuli zinazohusiana na siasa za MoHSW zilipiwe kutoka kwenye mfuko wa bunge.
- Wizara (MoHSW) iboreshe usimamizi wake wa fedha na kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inafikiwa/kupatikana.
- Mchakato wa bajeti uwe wazi zaidi kuhakikisha kuna ushiriki wa wadau wengine.

Muhtasari huu wa sera umeandaliwa na SIKIKA, mwanachama wa kikundi kazi cha bajeti cha Policy Forum.

Sikika ni asasi isiyokuwa ya kiserikali ambayo inafanya kazi ili kuwezesha wananchi kushirikiana vyema na watoa huduma ya afya kwa njia ya kuongeza ushiriki jamii,uwazi na uwajibikaji ndani ya sekta ya afya.

Policy Forum ni mtandao unaoshirikisha zaidi ya mashirika ya hiyari 100, yanayoshughulikia kupunguza umasikini, kuleta usawa na demokrasia, utawala bora na uwajibikaji.

Sikika

policy forum

Kitalu 270 Kiko Avenue Mikocheni B
S.L.P 38486 Dar es Salaam.
Simu: +255 22 2772611/+255 782 317434
Barua pepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum.or.tz